

HALMASHAURI YA WILAYA BAHU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: +255 26 2961400
Nukushi.: +255 26 2961401
Barua pepe: bahidc@gmail.com
Tovuti: www.bahidc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S. L. P. 2993,
Dodoma,
TANZANIA.

Kumb. Na. HW/W.10/40/25

Tarehe 14/06/2018

TANGAZO LA UHAKIKI KWA WATUMISHI WOTE

MKURUGENZI MTENDAJI (W) ANAWAARIFU WATUMISHI WOTE WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU KUWA "**ZOEZI LA UHAKIKI WA VYETI VYA KIDATO CHA NNE, SITA NA UALIMU**" LILISHAFANYIKA KWA MAELEKEZO YALIYOTOLEWA NA SERIKALI. AIDHA, KATIKA RIPOTI YA UHAKIKI KWA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU NA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UTUMISHI NA MISHAHARA ZINAONYESHA MAMBO YAFUATAYO:-

1. KUWEPO KWA WATUMISHI AMBAO TAARIFA ZAO ZA UHAKIKI HAZIPO KWENYE RIPOTI YA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUTOKANA NA KUHAMIA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU BAADA YA ZOEZI LA UHAKIKI KUPITA.
2. KUWEPO KWA WATUMISHI AMBAO WANAFANYA KAZI HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU KWA KUPATA UHAMISHO LAKINI MISHAHARA BADO HAJAHAMIA FUNGU LA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU.
3. KUWEPO KWA WATUMISHI AMBAO HAKUNA SEHEMU YOYOTE YA RIPOTI INAYOONYESHA KUWA AMEHAKIKIWA KWENYE KUNDI LA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU.

**KWA MAELEZO HAYO NAAGIZA MAMBO YAFUATAYO YAFANYWE HARAKA NA WATUMISHI HAO NDANI YA SIKU 10 KUANZIA LEO:
TAREHE 14/06/2018:-**

1. WATUMISHI WOTE AMBAO WAMEHAMIA BAHU BAADA YA ZOEZI LA UHAKIKI KUPITA NA KATIKA TAARIFA ZAO ZA UHAMISHO (SERVICE PARTICULARS) HAZIONYESHI KUWA WAMEHAKIKIWA “ **WALETE UTHIBITISHO WA MAANDASHI KUTOKA KWA MWAJIRI WA AWALI KUWA WALIHAKIKIWA NA UONYESHE MATOKEO YAKO KWENYE BATCH NAMBA NGAPI NA JINA LA MTUMISHI LIKO NAMBA NGAPI.**”
2. WATUMISHI WOTE AMBAO WANAFANYA KAZI HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU LAKINI MISHAHARA HAJAFIKA HALMASHAURI YA WILAYA BAHU BAADA YA KUPEWA UHAMISHO WALETE UTHIBITISHO WA MAANDISHI KUTOKA KWA MWAJIRI KUWA WAMEHAKIKIWA.
3. WATUMISHI AMBAO WANAONEKANA HAWAJAHAKIKIWA WALETE VYETI VYAO KWA AJILI YA UHAKIKI NA MAELEZO KWA NINI WALIKAIDI KUWASILISHA VYETI WAKATI ZOEZI LA UHAKIKI LINAFAANYIKA.


AIDHA, NAWAAGIZA WAKUU WA IDARA ZOTE NA VITENGO KUHAKIKISHA WATUMISHI WOTE WALIO CHINI YENU WAMEHAKIKIWA NA TAARIFA YA UHAKIKI HUO IWASILISHWE IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA KWA UFUATILIAJI. KWA AMBAO WANA UPUNGUFU ULIOORODHESHA HAPO JUU WATEKELEZE MAAGIZO YALIYOTOLEWA NDANI YA MUDA ULIOPANGWA NA SIO ZAIDI YA HAPO.

ANGALIZO:

WATUMISHI AMBAO WATASHINDWA KUTEKELEZA YOTE YALIYORODHESHA HAPO JUU MISHAHARA YAO ITASIMAMISHWA BAADA YA MUDA ULIOWEKWA KUISHA NA HATUA NYINGINE ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAO KWA MUJIBU WA KANUNI, TARATIBU NA SHERIA ZA UTUMISHI WA UMMA.

NAWATAKIA UTEKELEZAJI MWEMA

LIMETOLEWA NA


BERNADETHA K. JANUARY
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU.